



TAARIFA KWA UMMA

BENKI YA NMB YACHUKUA MALI NA MADENI YA CHINA COMMERCIAL BANK

Kama mnavyojua, Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, imeipa Benki Kuu ya Tanzania mamlaka ya kusimamia shughuli zote za benki na taasisi za fedha nchini kwa lengo la kuhakikisha uimara na uhimilivu wa sekta ya kibenki na ya fedha kwa ujumla.

Katika kutekeleza jukumu la usimamizi wa sekta ya fedha na kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 56(1) (g)(i |)&(iii) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, mnamo tarehe 19 Novemba 2020, Benki Kuu ya Tanzania iliamua kuiweka China Commercial Bank Limited chini ya usimamizi wake. Hatua hiyo ilichukuliwa baada ya Benki Kuu kubaini kuwa China Commercial Bank ina upungufu wa mtaji kinyume cha matakwa ya kisheria.

China Commercial Bank ilipewa leseni na kuanza kufanya shughuli za kibenki hapa nchini mwaka 2015, na kuwa mionganini mwa benki zenye ukuaji wa chini ulioisababishia hasara kwenye biashara kwa kipindi chote toka kuanza kutoa huduma za kibenki. Hadi kuchukuliwa na Benki Kuu, China Commercial Bank ilikuwa na mali zisizozidi Shilingi za Kitanzania bilioni 5. China Commercial Bank ilikuwa na tawi moja lililokuwa jijini Dar es Salaam.

Kabla ya kuiweka China Commercial Bank chini ya usimamizi wake, Benki Kuu ilifanya jitihada mbalimbali kuitia kwa wamiliki, bodi ya wakurugenzi na menejimenti ya benki kuwataka kuongeza mtaji kufikia kiwango kinachohitajika kisheria. Hata hivyo, pamoja na benki kupewa muda wa kutosha kutimiza matakwa hayo, jitihada hizo hazikufanikiwa.

Baada ya kuiweka chini ya usimamizi wake, Benki Kuu ilisitisha shughuli za utoaji wa huduma za kibenki za China Commercial Bank kwa muda wa siku 90 ili kuipa nafasi Benki Kuu kutathmini hatua za kuchukua ili kupata ufumbuzi wa suala hili.

Hivyo, Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuutarifu umma kwamba, kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 59 (4) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, mchakato wa kupata ufumbuzi wa tatizo la China Commercial Bank umekamilika baada ya kutathmini njia mbali mbali. Hivyo, kuanzia leo tarehe 4 Machi 2021, Benki Kuu ya Tanzania imeamua mali na madeni yote ya China Commercial Bank kuchukuliwa na benki nyingine kama njia ya ufumbuzi. Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 58(2)(h) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu imeamua kuhamisha kwa mujibu wa sheria (acquisition by operation of the law) mali na madeni ya China Commercial Bank kwenda NMB Bank Plc.

Kwa sasa, Benki Kuu, NMB Bank Plc na wadai wengine wanaendelea kuandaa taratibu za kisheria za kukamilisha mchakato wa uhamishaji wa mali na madeni ya China Commercial Bank Limited kwenda NMB Bank Plc. Wateja wenyewe amana na wadai wengine wa China Commercial Bank Limited watataarifiwa tarehe ya kuanza kupata huduma za kibenki kuitia NMB Bank Plc. Wateja wenyewe mikopo wanatakiwa kuendelea kulipa mikopo kulingana na mikataba yao.

Benki Kuu ya Tanzania inauhakikisha umma kwamba itaendelea kulinda maslahi ya wateja wenye amana katika mabenki kwa lengo la kuleta utulivu na uhimilivu katika sekta ya fedha.

Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki

botcommunications@bot.go.tz

4 Machi 2021